



SYRACUSE CITY SCHOOL DISTRICT

Jaime Alicea, Msimamizi wa Shule

Ofisi ya Msimamizi

Tarehe 12 Machi, 2020

Wapendwa Familia za SCSD,

Syracuse City School District inaendelea kufuatilia habari za hivi punde zinazohusiana na Virusi vya Korona (COVID-19). Afya na usalama wa wanafunzi, wafanyakazi na familia zetu ni kipaumbele cha juu na timu yetu yote ya usimamizi imekuwa ikijitahidi kuhakikisha kuwa tumejiandaa.

Kwa sasa, bado hakuna visa vilivyothibitishwa katika Kaunti ya Onondaga. Tunawasiliana mara kwa mara na Onondaga County Health Department (Idara ya Afya ya Kaunti ya Onondaga), Idara ya Afya ya Jimbo la New York (New York State Health Department, NYSDOH) na Kituo cha Kudhibiti Magonjwa (Center for Disease Control, CDC) na tutaendelea kufuata mwongozo wao.

Wiki hii, Gavana Cuomo alitangaza kuwa ikiwa mtu yeyote anayefanya kazi kwenye shule au mwanafunzi yeyote anayesoma shuleni atapatikana na virusi vya COVID-19 shule itahitajika kufungwa kwanza kwa saa 24. Hili litaruhusu wataalamu wa afya kuchunguza hali na kuamua hatua zinazofuata. Katika kipindi cha saa hizo 24 za mwanzo, shule itasafishwa na kuangamizwa viini kwa mujibu wa miongozo ya NYSDOH na uamuzi kuhusu siku ya kufunguliwa tena utatolewa baada ya hapo. Endapo tutaambiwa tunahitajika kufunga shule, tutakuarifu kupitia vyombo vya habari, kupitia mfumo wetu wa simu wa robo wa School Messenger na tutachapisha taarifa mtandaoni na kwenye mitandao ya jamii.

Mkurugenzi wetu wa Matibabu, Mkurugenzi wa Huduma za Afya na wauguzi mbalimbali wa shule walihudhuria mafunzo yaliyoandaliwa na maafisa wa afya wa karibu wiki hii. Mafunzo yaliangazia mkabiliano wa wauguzi wa shule endapo mwanafunzi au mfanyakazi atatambuliwa kama anayewezekana kuwa na COVID-19.

Ikiwa mtoto wako ana dalili kama za mafua (homa, kikohozi, kuhema) pendekezo kutoka kwa maafisa wa afya ni kumruhusu kukaa nyumbani. Ikiwa mtoto wako atakuwa na dalili hizi shuleni ni vyema amwone muuguzi wa shule ili kutathminiwa na muuguzi wa shule atawasiliana nawe baadaye.

Idara ya SCSD Teaching and Learning imekuwa ikijitahidi kukusanya taarifa za elimu ya wanafunzi endapo tutahitajika kufunga jengo kwa kipindi chochote. Tunataka kuwapa wanafunzi na familia shughuli za elimu ili kuendelea kujifunza sehemu zote za masomo wakiwa nyumbani. Shughuli ni nyongeza ya masomo ambayo watoto wenu hushiriki kila siku shuleni. Zitapangwa kulingana na kiwango cha daraja na somo. Pia tunajitahidi kutoa machaguo kadhaa ya masomo ya wanafunzi na familia zinazoweza kupata intaneti. Shughuli hizi za elimu na machaguo ya masomo ya mtandaoni vitachapishwa kwenye tovuti yetu, www.syracusecityschools.com/coronavirus.

Ikiwa una mtoto anayepokea huduma kupitia Special Education Department atatumia mkutano ujao wa mtoto wako wa Committee on Special Education (CSE) ili kupima huduma zozote ambazo alikosa na athari inayoweza kuwa nayo kwenye maendeleo ya mtoto wako endapo tutahitajika kufunga shule. Madarasa yetu yenye wanafunzi wadhaifu kiafya yanasafishwa vizuri na kufuatiliwa kwa karibu sana, kama tunavyojua kuwa wale ambao wana kingamaradhi yenye kasoro ndio walio kwenye hatari sana.

Mapema wiki hii, tulituma taarifa nyumbani tukiomba kuwa urekebishe taarifa zako za mawasiliano ikiwa unajua kuwa ulizibadilisha tangu mwanzo wa mwaka wa shule. Ni muhimu wakati wote kwa shule ya mtoto wako kuwa na taarifa za mwasiliani wa dharura za sasa kwenye faili.

Wilaya inafuatilia safari ya mwanafunzi na wafanyakazi ikiwemo maendeleo ya taaluma kwa wafanyakazi na michezo na mashindano ya elimu. Tunafuata agizo na mwongozo kutoka NYSDOH na kuangalia kila kitu kimoja baada ya kingine. Tutakuarifu endapo safari itafutiliwa mbali. Pia tunakagua vibali vyote vya jengo na matumizi ya umma ya majengo yetu.

Tafadhali kumbuka kuwa Virusi vya Korona vinafikiriwa kusambazwa kupitia mgusano wa mtu hadi mtu kupitia matone ya hewa iliyochafuliwa na mtu aliyeambukizwa kwa kukohoa na kupiga chafya. Hatua za kunawa mikono vizuri na usafi ni muhimu ili kuendelea kuwa na afya. Tunapodhibiti usambaaji wa virusi vingine, tunakuhimiza kuzungumza na mtoto wako kuhusu hatua zifuatazo za kuzuia:

- Nawa mikono yako mara kwa mara, haswa baada ya kuenda msalani na kabla ya kuandaa au kula chakula. Nawa kwa takribani sekunde 20 ukitumia sabuni na maji moto. Hakikisha kuwa pia umeosha ncha za vidole na sehemu za juu za mikono yako.
- Epuka kukohoa au kupiga chafya kwenye mikono yako au hewani. Jaribu kukohoa au kupiga chafya kwenye tishu, kisha uitupe wakati wote. Ikiwa huna tishu, kohoa/piga chafya kwenye mkono wako.
- Epuka kugusa macho, kinywa na pua yako.

Ikiwa una maswali au masuala yoyote tafadhali tembelea tovuti yetu kwa taarifa zaidi au wasiliana na Health Services Department kwa nambari 315-435-4145 au healthservices@scsd.us.

Wako Mwaminifu,



Jaime Alicea
Msimamizi wa Shule